

**ELIMU INAYOZINGATIA UMAHIRI
TATHMINI YA ELIMU YA SHULE YA JUNIOR
KAZI YA NOVEMBA–DISEMBA 2026**

DARAJA LA 8 – KISWAHILI

Muda: Saa 2

TAARIFA ZA MWANAFUNZI

Jina la Mwanafunzi: _____ **Jina la Shule:** _____

Nambari ya Tathmini: _____
Tarehe: _____

Msimbo wa Shule: _____ **Sahihi:** _____

MAAGIZO KWA WATAHINIWA

1. Andika jina lako katika nafasi iliyotolewa hapo juu.
2. Andika jina la shule yako na mkondo wako katika nafasi zilizotolewa.
3. Andika nambari yako ya udahili na tarehe ya tathmini katika nafasi zilizotolewa.
4. Karatasi hii ina sehemu mbili: **A na B.**
5. Jibu maswali yote katika **Sehemu A na Sehemu B.**
6. Jibu maswali kwa **Kiswahili.**
7. Majibu yote **LAZIMA** yaandikwe katika nafasi zilizotolewa kwenye karatasi hii.

USIONDOE ukurasa wowote kutoka kwenye karatasi hii ya maswali

Kiswahili - Grade 8 Opener Exams Term 3 2025 Set 3

Questions

1. **ZOEZI LA1: UFAHAMU**

Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu swali la 1 hadi la 5

Simba alikuwa amechoshwa na mizozo mingi kati ya wanyama. Alitoa amri wote wafike mkutano bila kukosa. Kila mara alitatusa unyanyasaji, vita, wizi na maovu mengine katika jamii ya wanyama. Mambo yalipokithiri ndipo akaamua kukiwahi chuma kingali moto. Ama kweli usipoziba ufa utajenga ukuta.

Adhuhuri mkutano ulianza rasmi. Hali ya chuki na hasira ilitawala wanyama wengine walionekana kiasi cha kulia. Hii ilitokana na maonevu waliyofanyiwa na wenzao. Yamkini wanyama hawakuelewa kuwa udugu ni kufaana bali si kufanana. Simba alijua kuwa hakuwa na budi ila kuwashauri na kutilia mkazo suala la kuishi kwa utangamano. Simba alitaka kujua chanzo cha uadui kati ya wanyama. Wacha pazuke ugomvi, lalama na ghasia nusura



uwe uwanja wa vita. Wanyama walilalamika kuwa kuna wale waliowala wana wao (kuku walisema mwewe hula vifaranga wao). Wengine walilalamika mashamba yao yaliharibiwa, vilevile kuna wale waliosema jamaa zao waliuliwa na kupoteza uhai.

Baada ya kusikiliza kwa utulivu, simba alijua alihitaji busara ili kutatua mizozo yote ya wanyama. Alianza kwa kusema hivi, "Wanyama wenzangu, katika dunia hii kila mmoja yu mbioni kutafuta maisha bora," hivyo basi hatuna budi kuishi kwa amani bila kumdhuru mwenzako, na iwapo kuna tatizo ambalo limetokea ni vyema kutatua kwa upendo na heshima. Tusiwe na ubinafsi na tamaa kiasi cha kutoyathamini maisha ya wenzetu. Kumbukeni kuwa umoja wetu ni nguvu yetu, la sivyo tutaangamia sote." Simba alikamilisha ushauri wake.

Wanyama wote hata wale waliokuwa wakizozana waliamua kuzika tofauti zao. Waliahidi mfalme wao kuwa wangeishi kwa amani, umoja na upendo.

Maswali

1. Kwa nini simba aliwaita wanyama mkutanoni? (alama 1)
2. Andika sababu yoyote iliyowafanya wanyama kuzozana. (alama 1)
3. Ni ushauri gani uliotolewa na simba kwa wanyama? (alama 1)
4. Kifungu '**waliamua kuzika tofauti zao**', kimetumia tamathali gani ya lugha? (alama 1)
5. Andika kwa kifupi namna unavyotatua mizozo na wenzako. (alama 1)

2. Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali

Serikali imepiga hatua katika kuandaa shule na taasisi ambazo zinawapa mafunzo watu wenye mahitaji maalum. Vilevile, kuna shule na taasisi za kiufundi ambazo zinasaidia baadhi ya watu walio na mahitaji maalum kama vile wasioona na wasiosikia ili kuwafunza ujuzi utakaowafaa katika maisha yao. Ujuzi huu ni kama vile useremala, ushonaji na uhandisi. Je, mna mchango gani katika kuwasaidia walio na mahitaji maalum miongoni mwenu?

Watu wenye mahitaji maalum wana vipawa vya kipekee. Wakipewa nafasi wanaweza kutoa mchango wao mkubwa katika jamii. Kuna wataalamu wa mitambo na tarakilishi wenye mahitaji maalum. Wakipewa fursa katika maisha watatumia vipawa vyao kujiimarisha na kuwasaidia wengine katika jamii. Ndio maana

tunasema kwamba, kuishi na ulemavu si kutojiweza bali ni kubarikiwa kwa njia tofauti na wengine. Ukweli ni kwamba, kuna baadhi ya mambo ambayo watu wenye mahitaji maalum huweza kuyafanya vyema.

Ni jukumu letu kama jamii kuwahudumia wenye mahitaji maalum bila kuwabagua ili wajisikie kamili kama binadamu wengine tusiwanyanyapae bali tuwaheshimu na kuwapenda.

Maswali

1. Andika ujumbe unaotokana na kifungu ulichokisoma. (alama 1)
2. Ni hatua gani iliyochukuliwa na serikali kuhusiana na watu wenye mahitaji maalum? (alama 1)
3. Ni watu gani wenye mahitaji maalum kulingana na kifungu ulichokisoma? (alama 2)
4. Kuishi na ulemavu si kutojiweza bali ni kubarikiwa kwa njia tofauti na wengine. Eleza kauli hii (alama 2)
5. Je, wewe unawasaidia vipi watu wenye mahitaji maalum? (alama 2)

3. **ZOEZI LA 2: UFUPISHO**

Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu swali la 11 hadi la 12

Uchafu wowote katika sehemu za umma huwa na athari tele kwa wakazi. Magonjwa anuwai kama kipindupindu, homa iletwayo na mbu na hata homa ya matumbo chanzo chake huwa ni uchafu. Magonjwa hayo huathiri watu kwa njia mbalimbali. Pamoja na athari hizo ni kutumia pesa nyingi katika matibabu, kukosa kufanya shughuli za kila siku na hatimaye kifo.

Ikumbukwe kuwa, mbali na usafi wa sehemu za umma na wa makazi yetu, ni vyema kudumisha usafi wa kibinafsi ambao hutuepusha na vimelea hatari, aidha hutupa utulivu na kutuepusha na magonjwa. Usafi wa akili na mawazo aidha ni muhimu. Tusiwaze mambo yanayotuletea athari hasi. Tuwe na mawazo chanya ili tuwe wastaarabu na wenye kutenda haki kwa kila mmoja.

Maswali

1. Andika habari kuu inayojitokeza katika aya ya kwanza. (alama 1)
2. Eleza kwa aya moja umuhimu wa usafi. (alama 2)

4. **ZOEZIL A3: SARUFI**

Soma kifungu kifuatacho kina nafasi 13 mpaka 17. Kwa kila nafasi umepewa majibu manne. Chagua jibu lifaalo zaidi.

Maadili ni tabia __13__ mienendo __14__ katika jamii. Hizi ni tabia __15__ zinakubaliwa na wanajamii __16__ hazikinzani na matarajio __17__. Mifano ya maadili ni upendo, heshima, uwajibikaji, umoja na mengineyo.

13. A. lakini	B. au	C. kwa hivyo	D. kwani
14. A. zinazokubalika	B. wanaokubaliwa	C. vinakubalika	D. inayokubalika
15. A. ambazo	B. ambao	C. ambalo	D. ambapo
16. A. kwa kuwa	B. wala	C. bali	D. kama vile
17. A. zao	B. lao	C. yao	D. kwao

5. **Kutoka swali la 18 hadi la 30, jibu kulingana na maagizo.**

Andika wingi wa sentensi ifuatayo. (alama 2) Mfuko ule wenye mkate na ndizi umechafuka.

6. Tumia kitenzi 'vua' kutunga setensi katika hali timilifu. (alama 2)

7. Mtoto wangu amefundishwa wenu walifaulu.

Andika neno lililopigiwa mstari ni la aina gani. (alama 1)

8. Unda sentensi ambatano kutokana na setensi hizi. (alama 2)

a. Amepimwa na daktari

b. Amepewa dawa na daktari

9. "Mwanafunzi alikuwa amemaliza mradi wake mwalimu alipofika." Sentensi hii ipo katika hali gani? (alama 1)

10. Tambua kitenzi kisaidizi katika sentensi.

(alama 1) Wanafunzi wangali wanasoma

Novela.

11. Chagua vivumishi vya kutoka kwenye orodha.

(alama 1) (wangu, yeye, mkubwa, hilo,


vibaya, watiifu)

12. Akifisha setensi ifuatayo.

(alama 1) tumenunua tarakilishi

kompyuta mpya

13. Chagua nomino za ngeli ya I-ZI kutoka kwenya kapu lifuatalo. (alama 2)



14. Andika sentensi ifuatayo katika hali kanushi.

(alama 1) Mwalimu akifika tutaanza
mashindano.

15. Ni kauli inayoonyesha maagizo kati ya hizi? Pigia mstari (alama 1)

- a. Ni vizuri kuhudumia wenye mahitaji maalum
- b. Chukua mzigo umpelekee jirani.
- c. Tunapenda kusoma Novela

16. Kamilisha maamkizi yafuatayo. (alama 2)

- a. Cheichei?
- b. Waambaje?

17. Andika setensi ifuatayo katika kauli ya kutendea.

(alama 1) musa alienda jikoni akapika chai.

18. **ZOEZI LA 4: FASIHI**

Taja aina mbili za nyimbo unazozijua. (alama 2)

19. Tofautisha kati ya mighani na visasili. (alama 2)

20. Tofautisha kati ya maudhui na dhamira katika tamthilia. (alama 2)

21. Tofautisha kati ya mandhari na ploti katika tamthilia. (alama 2)

22. Andika aina mbili za hadithi unazozijua. (alama 2)

23. **Andika insha ya kuvutia ukielezea**

ZIARA YANGU KATIKA SOKO

MAJIBU

1.
 1. Kutatua mizozo ya wanyama
 2. Vita, wizi, wanawao kuliwa, mashamba kuharibiwa.
 3. Aliwashauriwa kwa amani, upendo na heshima, waepuke ubinafsi na kuthamini maisha ya wenzao.
 4. Tashhisi / uhaishaji
 5. Tathmini majibu ya mwanafunzi
2.
 1. Kuwahudumia watu wenye manitaji maalum.
 2. Kuandaa shule na taasisi ambazo zinawapa mafunzo watu wenye mahitaji maalum.
 3. Wasioona na wasiosikia
 4. Watu wenye ulemavu, licha ya kuwa wana changamoto fulani, wakiwa nafasi na ujuzi wanaweza kufaulu.
 5. Tathmini majibu ya mwanafunzi
3.
 1. Kudumisha usafi wa sehemu za umma.
 2. Usafi wa sehemu za umma hutuepusha na maradhi, vimelea hatari, hutupa utulivu wa akili.
4. 13) au

14) inayokubalika

15) ambazo

16) wala

17) yao
5. Mifuko ile yenye mikate na ndizi imechafuka.
6. Hali timilifu huwa ni 'me' Tathmini sentensi. M.f. Mvuvi amevua samaki.
7. Kiwakilishi kimilikishi - wenu
8. Amepimwa na daktari na akapewa dawa.
9. Wakati uliopita hali timilifu.
10. Wangali
11. Mkubwa. watiifu
12. Tumenunua tarakilishi mpya.
13. Chupa, shingo, shule, meza
14. Mwalimu asipofika hatutaanza mashindano.
15. Chukua mzigo umpelekee jiran
16. a. Ewaa

b. Sina la kuamba
17. Musa alipikia chai jikoni
18. Nyimbo za kazi, nyimbo za kidini

19. Visasili ni hadithi ambazo huelezea chanzo fulani katika jamii ilhali mighani ni hadithi zinazohusu mashujaa. Huaminiwa kuwa ni mambo yaliyowahi kutendeka.
20. Maudhui ni mambo yanayozungumziwa katika kazi ya fasihi ilhali kuandika kazi ya fasihi. (Tamthilia)
21. Mandhari ni mahali mambo katika tamthilia hutokea nayo ploti ni mtirirko au mfuatano wa mambo katika kazi ya fasihi.
22. -visasili, hadithi fupi, mighani, Novela, riwaya, tamthilia
23. -

